**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS**

Menejimenti ya Utumishi wa Umma,
S.L.P. 2483,
Dar es Salaam.

Kumb. Na. C/AC/65/399/01

23 Februari, 2005

**WARAKA WA UTUMISHI NA. 2 WA MWAKA 2005**

**VIWANGO VYA MALIPO YA POSHO YA SIMU NA UMEME KWA VIONGOZI NA WATENDAJI WAKUU WENYE STAHILI YA KULIPIWA HUDUMA HIZI**

1. Tafadhali rejeeni barua zangu Kumbukumbu Na. C/AC/65/399/01/52 ya tarehe 21 Julai, 1999, C/AC/65/399/01 ya tarehe 24 Agasti 1999, na C/AC/665/399/01/105 ya tarehe 27 Septemba, 2002 kuhusu gharama za malipa ya posho ya simu na umeme kwa Viangazi na Watendaji Wakuu wenye stahili hizo.

2. Kutokana na kupanda kwa gharama zinazotolewa na Mashirika haya na kubadilika kwa miundo ya mishahara, Serikali imefanya marekebisho ya viwango vya units na posho.

3. Kwa mujibu wa mabadiliko hayo, posho hiza zitaendelea kulipwa kwa vigezo vya units za simu na umeme kwa mwezi. Aidha, viwango vipya vya units na posho vimeanyeshwa katika jedwali lifuatalo hapa chini.

**Viwango Vipya vya Units na Malipo ya Simu na Umeme**

| Kundi | Units za Simu kwa mwezi | Gharama Tshs. | Units za Umeme kwa mwezi | Gharama Tshs. |
|---|---|---|---|---|
| TGS. N - Q<br>LSS (J) 1 - 3<br>LSS (P) 1 - 6 | 650 | 110,000 | 1,480 | 170,000 |
| TGS. J - M | 450 | 70,000 | 1,290 | 150,000 |

**Tarehe ya Kuanza Kutumika:**

4. Waraka huu unaanza kutumika tarehe 1 Januari, 2005 na unafuta barua Kumbukumbu Na. C/AC/65/399/01/52 ya tarehe 21 Julai 1999, C/AC/65/399/01 ya tarehe 24 Agasti 1999 na C/AC 6 9/01/105 ya tarehe 27 Septemba, 2002.

J. A. Rugumyamheto
**KATIBU MKUU (UTUMISHI)**